# Learning by Ear 2012

## "Everyone's Different – Respect for Minorities"

## Episode 05

## Title: A Passion for Driving – A Woman in a Man's World in Uganda

**Author:** Leylah Ndinda

**Editor:** Katrin Ogunsade

**Proofreader:** Charlotte Collins

## List of caracters:

| ***Narrator*** | **male/female** | **about 35** | **english** |
|---|---|---|---|
| ***Stella Mary Nampijja*** Pronunciation: Stella Mary Nampidja (dj like in "Jazz") | female | 25 | english |
| ***Abbey Lulemiro*** Pronunciation: Abbey Lulemirò | male | about 40 | english |
| ***Anthony Wesaka*** Pronunciation: Anthony Wessacka | male | about 30 | english |
| ***Patience Atuhaire*** Pronunciation: Patience Atuha-i-re | female | about 35 | english |

**Intro:**

Hujambo na karibu katika sehemu ya tano ya kipindi chetu cha **Noa Bongo Jenga Maisha Yako** kuhusu jamii za watu walio wachache na jinsi wanavyokabiliana na ubaguzi barani Afrika. Wanawake si wachache bila shaka. Hata hivyo wanawake na wingi wao huo, mara nyingi hawapawi haki sawa na wanaume. Wanawake huwa hawana budi kupigania haki zao katika maeneo mengi duniani. Mara nyingi si rahisi wanawake kupata ajira. Leo tunakwenda Kampala, mji mkuu wa Uganda. Ni jambo la kawaida kupata wanawake wakiendesha magari barabarani. Lakini si kawaida kumpata mwanamke ambaye ni dereva wa gari la kampuni. Tumekuja kumshuhudia msichana ambaye amejikakamua vilivyo na kufikia hapo alipo.

**1. SFX environment**

## 2. Narrator

Ni siku ya Alhamisi alasiri yenye jua kali. Ni siku kama hizi ambapo mtu huhiari kujitosa kwenye dimbwi la kuogelea kuepukana na joto kali. Si watu wengi wanaomudu sampuli hiyo ya starehe. Wanapaswa kuwa kazini wakati huo.

Hakuna harakati nyingi zinazoendelea katika maegesho ya Kampuni ya magazeti ya Monitor huko Namuwongo, viungani mwa Kampala. Wanaume watatu na mwanamke mmoja wamekaa kwenye banda dogo wakipiga soga. Banda hilo linawafaa sana madereva wa Kampuni ya Monitor: limeezekwa mabati na hivyo linawakinga madereva hao na jua kali wakati wakisubiri kupewa kazi.

Ninakutana na Stella Mary Nampijja kwenye banda hilo.

Stella amezaliwa wa nne katika familia ya watoto watano. Ana umri wa miaka ishirini na mitano, (25) urefu wa futi tano na inchi tatu na rangi ya ngozi yake ni maji ya kunde. Ni mpole azungumzapo lakini anajiamini.

Stella alihitimu masomo ya Teknolojia ya Habari kutoka Chuo cha APTEC jijini Kampala. Lakini kwa nini akaamua kuwa dereva badala ya kufanya kazi aliyojifunza?

## 3. Soundbite Stella Mary Nampijja

*"Nilichagua udereva kwa kuwa ninapenda kuendesha magari. Kwa kweli ninapenda. Ninapenda kuendesha magari."*

**4. Narrator**

Stella anatoa tabasamu pale anapoelezea kilichomfanya auchangamkie udereva.

**5. Soundbite Stella Mary Nampijja**

*"Kilichonivutia kwenye udereva ni: wakati wangu mwingi wa faragha mimi huenda kutazama mashindano ya mbio za magari, kama madereva wengine. Ndio sababu nilivutiwa na udereva. Nilijua: Kweli nitaweza? Kwa hivyo, nikaamua niajiriwe dereva wa kampuni yoyote. Pengine siku za usoni nitashiriki mashindano ya mbio za magari."*

**6. Narrator**

Stella anasema kwamba mwanamke hapaswi kufa moyo anapokosa kupata kazi ambazo kwa kawaida husemekana ni za wanawake. Anasema alipohitimu masomo yake ya stashahada ya juu, aliona tangazo la kazi la Nation Courier nchini Uganda. Lilikuwa tangazo la kazi ya udereva katika kampuni ya magazeti ya Daily Monitor. Nation Courier ni tawi la Kampuni ya Habari ya Nation Media Group, ambayo ina magazeti na vituo vya redio na televisheni katika Afrika Mashariki na Kati.

Stella aliwasilisha barua yake ya maombi lakini hakupata majibu kwa kiasi miezi mitatu. Siku moja akaitwa kutathiminiwa. Msimamizi wake Abbey Lulemiro anazungumzia utendakazi wake.

**7. Soundbite - Abbey**

*"Alifaulu, aliwashinda wanaume. Kwenye awamu ya mahojiano ya mazungumzo, alishika nafasi ya nne na tulikuwa tukihitaji madereva wanane. Hivyo ndivyo alivyoajiriwa."*

**8. Narrator**

Lulemiro anakumbuka jinsi madereva na wafanyakazi wengine walivyohisi walipoambiwa kwamba kampuni hiyo ilikuwa imemwajiri dereva mwanamke.

**9. Soundbite Abbey**

*"Habari hizo ziliwasisimua wengi wao. Walisema, ' Wamemleta mwanamke, wamemwajiri msichana.' Watu wote walichangamka. Walitaka kuona sana huyo dereva mwanamke akifanya kazi. Kweli ana uwezo wa kuendesha gari? Kwa sababu tuna imani kwamba mwanamke hawezi kuendeshagari yenye gia za mikono. Watu wengi walitaka kufanya kazi wakati wa zamu ya huyo dereva mwanamke ili wahakikishe kweli kwamba huyo mama aliimudu kazi yake barabarani. Katika hali hiyo wamekuwa wakimsaidia sana kazini mwake."*

**10. Narrator**

Stella anaridhia anavyotendewa na madereva wenzake wanaume.

**11. Soundbite- Stella**

*"Madereva wetu wanaume wananitendea vyema kwa kuwa mimi ndiye dereva mwanamke pekee. Wao hunisaidia ninapotatizika. Naam, wananitendea vyema."*

**12. Narration**

Stella amekuwa kazini hapo kwa kiasi cha miezi mitatu kufikia sasa. Ndiye dereva pekee mwanamke anayefanyia kazi Nation Courier nchini Uganda. Kazi yake ni kuwapeleka na kuwarejesha wanahabari wanapotumwa kutafuta habari. Aidha, anafanya kazi ya kusambaza magazeti na mizigo katika maeneo mbali mbali nchini Uganda.

**13. Soundbite Stella**

*"Si rahisi kwa mwanamke kuendesha gari. Kwa mfano katika kitengo changu hupumziki. Watakwambia uwapelekee wahariri Kasangati, kutoka Kasangati hupumziki bali unaambiwa upeleke mwanahabari Mulago. Unampeleka kisha unarejea. Ni kazi inayochosha. Lakini ninaipenda. Ninaipenda kazi yangu."*

**14. Narration**

Stella anasema anaweza tu kuendesha gari kasi kilomita mia moja na ishirini kwa saa. Hajakumbana na mikosi mingi barabarani. Changamoto kubwa kwake ni msongamano wa magari, na barabara mbovu zinazomfanya kupunguza kasi. Anafahamu fika kwamba ni muhimu kuzingatia wakati hasa kwa wanahabari, kwa hivyo huingiwa na wasiwasi magari yanapokwenda polepole kwani wanahabari hao huweza kuchelewa wanakokwenda.

Hata hatujamaliza kumhoji Stella tunaona watu kadhaa wanaomsubiri awapeleke kazini. Msimamizi wake Abbey Lulemiro anampa kazi nyingine.

**15. Soundbite Abbey**

*"Stella,mpeleke huyu bwana. Anakwenda Bugolobi kwenye Kampuni ya Ulinzi ya KK."*

**16. *SFX- Stella starting her car and driving off***

**17. Narrator**

Stella sasa ameshaondoka. Tunatumia fursa hii kuzungumza na baadhi ya wanahabari ili watupatie maoni yao kuhusu kazi ya Stella.

**18. Soundbite - Male reporter - Anthony Wesaka**

*"Nimjuavyo mimi, yeye huzingatia taa za barabarani, hapiti magari ovyo ovyo jinsi madereva wanaume wanavyofanya. Kwa vile kuna magari mengi mjini, dereva akiharakisa huenda akasababisha ajali. Si sawa kwetu sisi kwa kuwa tunataka kuharakisha tupate habari ilhali yeye anaendesha gari taratibu. Hata hivyo, jambo muhimu zaidi ni hilo la kuwasili wendako salama u salimini. Bora kufika huko salama kuliko kupata majeraha ya ajali kwa sababu ya kwendeshwa kwa kasi."*

**19. Narrator**

Mwanahabari, Patience Atuhaire, anakumbuka mara ya kwanza kupanda gari lililoendeshwa na Stella.

**20. Soundbite - Female reporter - Patience Atuhaire**

"Mara yangu ya kwanza, alinipeleka Makerere, na kabla hajaondoka, akaniuliza iwapo nilitaka anisubiri. Hilo halikuwa jambo la kawaida kwa madereva wa kampuni ya Monitor. Mimi nilimwambia, "Acha niulizie muda nitakaotumia, kisha nitakuarifu." Nilirejea kwake nikampasha niliyompasha, naye akaondoka. Alikuwa na subira. Hakulalamika wala kusingizia kwamba alikuwa akihitajika afisini."

***KW begin***

**21. Narrator**

Lau wangekuwa wao ndio waamuzi, je hawa wanahabari wangehiari dereva mwanamume au Stella?

**22. Soundbite - Anthony Wesaka**

*"Tukizingatia sekta yetu hii ya habari, bora nikamteua dereva mwanamume kwasababu mambo ya habari yanahitaji mtu wa kasi. La sivyo huenda ukakosa habari. Ikiwa ni mpiga picha, huenda asipate kupiga picha za matukio. Kwa hivyo, ningehiari madereva wanaume. Lakini mimi nimo kwenye kitengo cha biashara wala sina kazi nyingi. Kwangu mimi sasa hivi bora Stella, kwa kuwa anaendesha gari kwa makini na anazingatia sheria za barabarani."*

**23. Soundbite - Patience Atuhaire**

*"Ningemchagua yeye. Kwa vile ni mwanamke nadhani ana imani ya mama kwa mwanawe. Hasa unapomweleza: Tunahitaji habari hii na hatuna budi kuishughulikia ipasavyo. Au: Ukitaka kuondoka, uniarifu ili nijue namna nyingine ya kurejea ofisini."*

***KW end***

**24. Narrator**

Katika mataifa mengi barani Afrika, wanawake hukumbana na ubaguzi kazini na pia shuleni. Lakini nchini Uganda mambo si mabaya sana kwa wanawake.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo nchini Uganda, suala la usawa wa jinsia limekuwa likishughulikiwa tangu mwaka 1990 ambapo wanawake wanazingatiwa sana wakati wa wanafunzi wanapojiunga na vyuo vikuu na taasisi nyingine za elimu ya juu. Wanawake huongezewa alama (pointi) za ziada wanapopeleka maombi ya kujiunga na vyuo. Sera hiyo imesaidia kuongeza idadi ya wanawake wanaojiunga na vyuo vikuu.

***KW begin***

Katiba ya Uganda pia imesaidia kuimarisha hali za kina mama katika ngazi zote, hata kwenye uongozi. Mathalan, kila wilaya nchini Uganda ina mwakilishi mwanamke ambaye jukumu lake kuu ni kushughulikia masuala yanayowaathiri wanawake katika eneo lake.

***KW end***

Wanawake wengi wanahitimu kutoka vyuo vikuu na taasisi nyingine za elimu ya juu. Kwa hivyo, ni nadra sana kusikia wanawake wakilalamika kwamba wanabagulia kwa sababu ya jinsia yao. Pengine hii ndiyo sababu Stella hatatiziki kufanya kazi pamoja na wanaume.

Msimamizi wake Abbey Lulemiro anamsifu.

## 25. Soundbite Stella's Boss - Abbey Lulemiro

*"Ni mwanamke mchapa kazi, ana bidii kazini, na anapenda kuendesha magari. Kwa sababu alipokuja mimi nilidhani- na hata nilimuuliza hilo swali wakati wa mahojiano- alikuwa akitaka kazi ya udereva au alitaka kutumia fursa hiyo kupata nafasi nyingine katika idara nyingine. Alisema, 'Hapana, japo nifanye kazi nyingine, nimekuja hapa kuendesha magari. Ninapenda kuendesha magari.' Nilimuuliza ni kazi gani nyingine ambayo anaweza kufanya akaniambia ni kazi ya data. Mara nyingine mimi humpa hiyo kazi ya data kwa sababu anaifahamu. Wakati kazi ya udereva inapopungua yeye huja hapa ofisini kunisaidia."*

## 26. Narrator

Ijapokuwa Stella amehitimu masomo ya Habari na Teknolojia, anasema hadhani kwamba atajiendeleza zaidi kwenye masomo hayo. Anasema sasa hivi anaridhia zaidi kuendesha magari. Anatumai atakuwa dereva wa mbio za magari siku za usoni.

## 27. Soundbite- Stella

*"Kuendesha magari ni kazi nzuri kwa sababu mtu hutembelea sehemu nyingi asizozijua na pia huwa na fursa ya kutangamana na watu. Mimi najipatia riziki na kazi hii ya udereva lakini pia ninaiependa sana."*

**Outro:**

Tunatumai kwamba umevutiwa kusikiliza kisa hiki cha mwanamke dereva kutoka Kampala nchini Uganda. Mwandishi wetu alikuwa Leylah Ndinda. Ukitaka kusikiliza tena sehemu hii, au visa vingine vya jamii za watu walio wachache na jinsi wanavyokabiliana na ubaguzi barani Afrika, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw.de/lbe. Usikose kututegea sikio kwenye sehemu ijayo. Kwaheri!